

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
11 Aprili 2009**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Athumani Mussa Kitemo
Bashiri Rashidi
Edward Marline
Elaine Baker
Elia Kimena
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Kibwana Mohammad Msiga
Mejah Mbuya
Mohammed Samwely
Paulo Atibu Hatibu
Saidi Brashi
Shamte J Kigoma

Kongamano / JICA

Edgar hakuwepo kwenye mkutano kutoa repoti kuhusu JICA. Juma atafuatalia wiki hii kujaribu kupata mkutano na JICA.

Mradi wa Wamba

Una Osili alitumia email kusema anashughulika kupata document kuonyesha kwamba transfer imetumikwa.

Wanachama waliomba Elaine asafisha photos za mafunzo ya Kigamboni kwa ajili ya bao ya tangazo.

Ruzuku ya Foundation for Civil Society

Bado Elaine anafuatalia CVs za waalimu wa kompyuta.

Ushirika wa Fast Cycle couriers

Tunahitaji barua ya kujitambulisha kwa kata kabla ya wao kupiga mihuri kwenye barua yetu kuhusu ushirika. Elaine ataandaa barua na kumpa Juma.

Video ya usalama wa baisikeli

Elaine alileta DVDs sita pamoja na stika. Baadhi ya wanachama wataenda nazo kupima na watarudisha. Elaine atatengeneza CDs pia na atatengeneza DVDs zingine ambazo Mejah alichangia. Sanduka la stika za CD 100 zina gharama ya Tsh 36,000 na zipo duka la Masumin, mtaa Jamhuri. Edward atatafuta bei za kununua kiasi ndogo zaidi, na pia bei za DVD na CDs.

Wimbo

Elia aliimba wimbo wake tena kwa ajili ya watu ambao hawakuwepo wiki jana. Elia ataenda na Mejah kwa Ramali, Fish club Ilala recording studio kuandaa single.

Mkutano wa WHO wa usalama barabarani

WHO wametumia barua ya kumwalika Mejah. Atafuatalia kupata visa ya Ubeljiji.

Re-cycle

Mejah aliongea na mtu TRA ambaye alisema inawezekana kupata samaha ya kodi kwa NGOs. Elaine aliandika barua kwa TRA kuomba taarifa kuhusu taratibu kupata samaha. Mejah atafuatalia wiki hii.

Kiingereza

Wanachama waliojiandikisha kusoma kiingereza hawahudhuria sana kwa sababu muda ya saa saba mchana siku za wiki ni ngumu kwao. Tulikubali darasa ziwe mbili kwa wiki – baada ya mkutano wa UWABA na saa kumi mchana siku za jumapili.

Mambo ya hela na guta

Ramadhan alitumia Tsh 14,000 ya hela ya guta kwa kupitia Bashiri na anadaiwa Tsh 7,000. Posho ya Juma ya mwezi wa tatu ya Tsh 20,000 ililipwa. Juma sasa ana Tsh 15,000 ya hela ya UWABA.

Mambo mengine

Tulikubali kuandika barua kwa Vodacom kuwapongeza kwa kuweka bao la tangazo mkoani kuhamasisha usalama barabarani, na pia kusema dereva waheshimi wapanda baiskeli.

Edward atakuja na kamera yake ili kusaidia katika kutengeza vitambulisho vya wanachama wapya.